TANGAZO LA SERIKALI Na. 40 la Tarehe. 24/1/2025

SHERIA YA USIMAMIZI NA TOZO YA USHURU
(SURA. 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA GARI MOJA LINALOINGIZWA NCHINI NA WAWAKILISHI WA SHIRIKA LA WAKIMBIZI DUNIANI NCHINI TANZANIA YA MWAKA 2025

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Gari Moja linaloingizwa na Shirika la Wakimbizi Duniani nchini Tanzania ya mwaka 2025 itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 31 Oktoba, 2024.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha Ushuru wa Bidhaa kwa Gari Moja kinachotakiwa kulipwa kuhusiana na yaliyoainishwa kwenye jedwali, linaloingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali cha forodha na Shirika la Wakimbizi Duniani umesamehewa.

Masharti

3. Msamaha wa kodi unaotolewa chini ya Amri hii utafika ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba msamaha chini ya Amri hii haukutolewa, iwapo gari husika litatumika kwa matumizi tofauti au litahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote atapewa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Kuisha kwa muda

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafika Ukomo tarehe 31 Machi, 2025.

JEDWALI

*(Imetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| SN | Maelezo | Mwaka | Namba ya Injini | Idadi | Namba ya Chassis | Mahali |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Land Cruiser, hard top converted to Ambulance Model year 2023, White Colour, | 2023 | 1HZ1061729 | 01 | JTERB71J30F027283 | limeingizwa |

Dodoma,
30 Disemba, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*